



Bi. Cheryl Watson-Harris, Superintendent

Bi. Vickie B. Turner, Mwenyekiti wa Bodi  
 Bw. Dijon DaCosta, Mwenyekiti Msaidizi  
 Bi. Anna Hill  
 Bw. Marshall D. Orson  
 Bi. Deirdre Pierce  
 Bi. Allyson Gevertz  
 Dkt. Joyce Morley

## INAPASWA KUCHAPISHWA BILA KUKAWIA

Jumanne, 12 Januari 2021

## Mawasiliano:

Portia Kirkland, 678-427-4898  
 Carla Parker, 404-734-1717

## Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb Kuchelewisha Kufungua Shule Tena

STONE MOUNTAIN, Ga. – Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb (DCSD) inachelewesha kurudi shuleni. Wanafunzi hawatarudi kwa masomo ya ana kwa ana mnamo Januari 19.

Msimamizi wa DCSD, Cheryl Watson-Harris na timu yake wamewasilisha mpango uliosasishwa wa kufungua tena wa Wilaya katika mkutano wa Bodi ya Elimu wa Januari 11. Maamuzi yalitolewa kwa umakini kwa kuzingatia hali ya COVID-19 na shule kukomesha mafunzo na elimu.

Taarifa ya wiki mbili itashirikiwa na familia kabla ya tarehe inayotarajiwa ya kurudi kwa wanafunzi katika masomo ya ana kwa ana. Wilaya italenga kutekeleza mikakati ya kupunguza hatari na utayari wa shule. Operations itaendelea kutekeleza ukaguzi wa sehemu tano muhimu za matayarisho ya shule:

- Bidhaa za Kujikinga (PPE) na Bidhaa za Usafi
- Usambazaji wa Bidhaa za Usafi na Taratibu
- Kukaa Mbali na Wengine na Kupanga Nafasi
- Kupata Maji
- Mabomba na Mifumo ya HVAC
- Ishara za Usalama za COVID-19 shuleni

Kipaumbele ni kuhakikisha kwamba wafanyakazi na wanafunzi wote wako salama kusoma na kufanikiwa katika majengo yetu ya shule ya DCSD. Hii itajumuisha pia kufuatilia mikakati mitano muhimu ya Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa ya kupunguza zaidi viwango vya hatari vya COVID-19 kama vile:

- Matumizi sahihi na ya mara kwa mara ya barakoa
- Kutokaribiana na watu ikiwa inawezekana
- Kunawa mikono
- Kusafisha na kuuva vidudu
- Kuwafuatilia watu waliokaribiana kwa kushirikiana na Bodi ya Afya ya DeKalb

Wilaya itakuwa na mkutano wa mtandaoni wa Town Hall na Msimamizi Watson-Harris mnamo Alhamisi, Jan 14, 2021 kuanzia saa 6 hadi 7 p.m.

Kwa maelezo ya ziada kuhusu mpango wa kufungua shule tena, tembelea [www.dekalbschoolsga.org/school-reopening](http://www.dekalbschoolsga.org/school-reopening).